

27 Agosti, 2024

TAARIFA KWA UMMA

1. Baraza la Uongozi wa Chama cha Wanasheria Tanganyika tunaendelea kufuatilia kwa karibu mgogoro kuhusiana na changamoto za kidemokrasia, kiutawala na haki ya kuishi katika maeneo yao ya asili na haki ya ulinzi wa mali kwa mwananchi kwa mujibu wa Ibara ya 26 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria kwa jamii ya Kimasai katika Tarafa ya Ngorongoro.
2. Tumefurahishwa na hatua za Jeshi la Polisi kutotumia nguvu dhidi ya maandamano ya wananchi wa Ngorongoro kudai haki yao na zaidi tunawapongeza wananchi wa jamii ya Kimasai waishio Ngorongoro kwa kutumia haki yao na umoja wao kuandamana kwa amani kwa kusudi la kudai haki zao za kikatiba na kisheria.
3. Katika tamko letu la awali kuhusu malalamiko ya wananchi wa jamii ya Kimasai wa Ngorongoro pamoja na mambo mengine tulitoa wito kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kurejesha huduma zote za kijamii zilizoondolewa kwa wakazi wa Ngorongoro hususan Wamasai pamoja na kusitisha tangazo la amri ya kufuta baadhi ya vijiji ambalo kwa kiasi kikubwa liliathiri Tarafa ya Ngorongoro.
4. Tunaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua za awali kwa kutuma mawaziri waandamizi na kuzungumza na wananchi pamoja na tamko lake kupitia maelezo ya Mawaziri husika la kurejeshwa kwa huduma za kijamii zilizositishwa katika eneo la Ngorongoro na tamko lake la kuridhia kusitishwa kwa tangazo la kufuta vijiji na vitongoji katika eneo la Tarafa ya Ngorongoro na kutangazwa kuanza zoezi la uboreshaji kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Aidha Tunapongeza tamko la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mh. Rais Dr. Samia Suluhu Hassan** la kukutana na wawakilishi halali wanaotokana na mapendekezo ya wananchi wa jamii ya Kimasai wa Ngorongoro.
5. Hii ni dalili njema kwamba rai na wito wa wananchi wa Ngorongoro pamoja na taasisi nyingine zote za kijamii, kitaaluma, kidini na kisiasa zenye mapenzi mema na taifa letu umezingatiwa kwa sehemu jambo ambalo ni hatua njema.
6. Tunatoa wito kwa vyombo vya dola hususan Jeshi la Polisi kuhusiana na suala hili la Ngorongoro kuhakikisha vinatumia weledi na kuacha kuwabughudhi viongozi wa harakati za wananchi wa Ngorongoro kwa kuacha vitisho vya kuwakamata au kuwatafuta kwa namna inayoweza kuharibu utulivu na maendeleo makubwa yaliyoanza kupatikana kuhusiana na mgogoro huu.

7. Aidha tunapenda kuujulisha umma pia Kamati ya Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) kuhusiana na sakata la ardhi na uwekezaji ilikwisha undwa na kuanza kazi na kwamba inaendelea na majukumu yake kwa kusudi la kupata namna bora ya kuishauri Serikali na kuhakikisha upatikanaji wa suluhisho jumuishi na la kudumu kuhusu uwekezaji, uhifadhi, ulinzi wa haki na hadhi ya wana jamii katika maeneo mbalimbali ya nchi inapatikana. Jukumu hili TLS inalolifanya ni kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria ya Chama cha Mawakili Tanganyika, Sura ya 307.

Imetolewa na Baraza la Uongozi la Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS).



Boniface A.K Mwabukusi

Rais